



REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

SECOND ASSEMBLY –FOURTH SESSION

THE HANSARD

Monday, 10th February 2020

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 2:30 p.m.*

[The Speaker (Hon. Kahindi) in the Chair]

PRAYERS

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

QUERIES TO THE COUNTY EXECUTIVE COMMITTEE MEMBER FINANCE

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Members, the office of the Speaker is in receipt of questions that have been raised by hon. Members to the County Executive Committee Member (CECM) Finance. The first question is from hon. Kiraga directed to the Committee on General Oversight. The Subject is on the implementation of the approved County Budget.

“The above subject matter refers. As you may be aware, on the 4th Day of December 2019, the County Assembly of Kilifi passed the County Supplementary Appropriation Bill, 2019, so as to cater for pending bills and appropriate for additional equitable share from the County Allocation of Revenue Act, 2019.

As you may further be aware, the CECM in charge of Finance and Economic Planning submitted another Supplementary Appropriation Proposal to the county assembly on the 31st of January, 2020, for the House to appropriate for other pending bills and misplaced funds in the Kilifi County Supplementary Appropriation Act, 2019. The CECM in charge of Finance and Economic Planning has not yet furnished the County Assembly with the County Budget Implementation Report for the period July 2019 to December 2019.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Pursuant to Standing Order 42, I request that you refer the matters raised in this question regarding the County Budget Implementation Report to the Committee on General Oversight established in Standing Order 153.

I further request the CECM in charge of Finance and Economic Planning be invited before the Committee on General Oversight with all the officers, papers, books, documents and records related, to give further clarifications and inform the assembly on the matters raised in this question.”

Hon. Members, I have considered the questions; they are eligible in law and I therefore direct that the Office of the Clerk calls for a letter to be written to the CECM to appear before this House on Wednesday 19th February, 2020.

QUERIES TO THE COUNTY EXECUTIVE COMMITTEE MEMBER EDUCATION

The second question is raised by hon. Mramba to the CECM Education.

“As you may be aware during the Special Sitting on the 15th day of January 2020, the County Assembly of Kilifi unanimously passed the Kilifi County Ward Scholarship Fund Amendment Bill, 2020.

As you may also be aware, the Kilifi County Ward Scholarship Fund Act, 2018 provides for the administration of Ward Scholarship Fund by the Board to ensure timely and efficient disbursement of funds to the qualifying beneficiaries and institutions.

Noting with concern, there has been confusion with regards to the disbursement of funds to the beneficiaries, where the Ward Scholarship Fund Board has been managing the funds in a hazardous manner. This has resulted to the beneficiaries getting stranded due to lack of communication between the Ward Scholarship Fund Board and the Ward Scholarship Committee.

Pursuant to Standing Order 42, I do request that you refer the matters raised in this question regarding the implementation of the Ward Scholarship Fund to the Committee on General Oversight established in Standing Order 153.

I further request that the CECM in charge of Education and ICT and the Chief Officer in charge of Education and ICT in his capacity as the Chairperson of the Ward Scholarship Fund Board be invited before the Committee on General Oversight with all the officers, papers, books, documents and all records related to give further clarifications and information to the assembly on the matters raised in this question.”

Hon. Members, I have also considered the questions raised as required of me by the Standing Orders, the same stands approved. The Office of the Clerk is to cause a letter to be written to the relevant offices to appear before the House on the same date of Wednesday 19th February, 2020.

Hon. Members, following the matters raised by the Leader of Majority, it has been deemed wise that all Members who have issues on education development, to please forward their issues to the office of the Principal Clerk so that on Wednesday a general letter regarding the same can be sent. It has been realized that there are so many development queries that need to be answered by the CECM.

Hon. Mwarandu: Thank you so much Mr. Speaker for this opportunity. In 1988 I was admitted in class one and in 1989 the famous *maziwa ya nyayo* started and am a fully beneficiary of the scheme. I am assuming that most of the hon. Members here are also beneficiaries. Though

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

it may not be in the Standing Orders, I would like to request that we all observe a minute of silence before anything else.

Hon. Hassan: Asante sana Bw. Spika kwa nafasi hii. Yale aliyoyazungumza mheshimiwa pale ni ya ukweli. Ingekuwa bora Bunge hili kwa heshima zote lihudhurie mkutano wa kesho kule Nairobi kumsindikiza Baba wa Taifa. Nikimalizia, nina ombi kuhusu maswala ya elimu; kumekuwa na sintofahamu fulani kwa hivyo nilikuwa naomba kama itawezakana tuwe na Kamkunji tuweze kutatua swala hilo. Asante sana.

The Speaker (Hon. Kahindi): Let us all rise and observe a minute of silence for the departed soul of the second president of the Republic of Kenya Daniel Toroitich Arap Moi.

(Members stood and observed a minute of silence)

Thank you hon. Mwarandu for bringing that to our attention. I cannot speak about going for the burial tomorrow; however let us proceed to the next Order.

PROCEDURAL MOTION

APPROVAL OF HOUSE BUSINESS COMMITTEE MEMBERSHIP

The Leader of Majority (Hon. Mwachethe): Thank you Mr. Speaker. I would like to move a Procedural Motion on the approval of Members to the House Business Committee.

THAT, Pursuant to the provisions of Standing Order 151, Sub Clause 1 (f), this Assembly approves the following 7 other Members to the House Business Committee in addition to the Members specified under Standing Order 151 (1) (a, b, c, d and e). The Members to be approved are Hon. Peter Ziro Ngowa, Hon. Jana Tsuma Jana, Hon. Christopher Mwambire, hon. (Ms.) Victorine Atieno Nyamolo, hon. (Ms.) Mary Anzazi Maneno, hon. (Ms.) Saumu Sidi Julius and hon. Daniel Kitsao Charo. Thank you, Mr. Speaker. I ask my Chief Whip to second.

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, hon. Mwayaa.

Hon. Mwayaa: Mheshimiwa Spika wacha kwanza nimpongeze Kiongozi wa Walio Wengi Bungeni kwa kuleta majina haya. Kuna haja tuwe na majina haya tena katika Bunge hili ili tunapopanga kazi zetu za Bunge tuwe tuna hawa watu. Hawa watu wamefanya kazi katika Bunge hili vizuri na ikawa ni wazi wakaweze tena kuregeshwa katika sehemu zao za kazi na tukaweze kupanga kazi nzuri ambayo inanza mwaka huu. Mheshimiwa Spika, nampongeza Kiongozi wa Walio Wengi na nafikiri hawa watu ambao majina yao yameregeshwa ni kulingana na kazi yao nzuri waliyoifanya. Nawaunga mkono. Asante.

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes hon. Pascal, what is the Point of Order?

Hon. Pascal: Asante Mheshimiwa Spika kwa nafasi ambayo umenipatia ingawaje mheshimiwa ambaye alikuwa kwa Sakafu amekaa lakini nilikuwa nataka atueleze ni watu gani anazungumzia katika Mswada huu ambao tunajadili. Wale tunaazungumzia hapa ama wale ambao wameandikwa katika orodha kwenye karatasi hii ni waheshimiwa; sasa sijui nasikia watu ...mheshimiwa angetueleza vizuri ni watu wapi ili tuweze kujua. Asante.

The Speaker (Hon. Kahindi): I understand. This is just a procedural thing just to confirm but they are hon. Members. Looking at the HANSARD one will think that we introduced new people. It is well noted hon. Pascal. Yes, hon. Stanley (Kenga).

Hon. Kenga: Shukran sana mheshimiwa Spika kwa nafasi ambayo umeweza kunipa ili niweze kuchangia Hoja ambayo iko mbele yetu. Nataka niseme kwamba viongozi hawa ambao

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

wameteuliwa kutoka kwa vyama mbali mbali ili waweze kukamilisha kamati, ni viongozi ambao wako na nafasi nzuri sana ya kuweza kusaidia Bunge hili endapo wataungwa mikono kikamilifu ili tuweze kuendesha shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, wakati tunauliza tuweze kukubali na kupitisha Hoja hii ya majina haya ili yaweze kuingia katika kamati, nataka nitambue kwamba kwa sasa tuko katika majonzi. Taifa letu la Kenya linaomboleza kumpoteza aliyekuwa Baba wa Taifa ambaye kwa muda wa miaka 24 aliweza kuongoza Taifa letu la Kenya.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba wakati Rais wa Jamhuri Daniel Toroitich Arap Moi alipokuwa mamlakani, hata ungeuliza mkenya yeyote Rais wa Uganda anaitwaje angekwambia ni Moi. Katika fikra za wananchi waliweza kujua tu Rais ndani ya ulimwengu huu bila kuangalia ni nchi gani Moi alikuwa anaongoza; hii ni kwa sababu aliweza kukaa katika uongozi kwa muda mrefu.

Labda tutauliza pia viongozi ambao waliweza kuteuliwa wajitoe kikamilifu ili waweze kufanya majukumu yao vizuri ili pia katika historia tuweze kuwakumbuka kwamba wakati mheshimiwa Peter Ziro, mheshimiwa Jana Tsuma Jana, Christopher Mwambire, Victorine Atieno Nyamolo, Mary Anzazi Maneno, Saumu Sidi Julius na mheshimiwa Daniel Kitsao walipopata nafasi ndani ya Bunge hili waliweza kufanya kazi kwa uzuri na kuweza kupeana mwelekeo ambao ni mzuri.

Mheshimiwa Spika itakumbukwa kwamba mara nyingi Bunge hili limekosa biashara; limekosa kazi ya kufanya kwa sababu ati hakuna Hoja wala Miswada ambayo waheshimiwa wanaleta. Ndio maana nikauliza ni vizuri wakati tunawapitisha pia tuweze kuwaunga mikono kuhakikisha kuwa kila mmoja anawajibika kikamilifu katika maswala yake.

Niseme tu mheshimiwa Spika, nashukuru kwa mwelekeo ambao umepeana kuwa tuweze kupeana heshima lakini vile vile niseme mawazo yaliyotoka kwa mheshimiwa wa Matsangoni ni mawazo mazuri. Nadhani ndani ya taifa hili itakuwa hatujafanya jambo la busara endapo hatutapata nafasi kama Bunge kuenda kuwakilisha kikamilifu na kuonekana.

Kaunti ya Kilifi ni sura ya Kenya na sisi viongozi Wajumbe ndani ya Bunge letu ni wawakilishi wa wananchi katika Taifa la Kenya. Sasa sijui itakuwa vipi endapo kuna watu wanaomboleza na Kilifi ikose uwakilishi; sura ya Kilifi itakuwa vipi? Nadhani tuna nafasi na hatujachelewa bado tunaweza kukaa na kujipanga kuona ni vipi kama Bunge la Kilifi tutapata nafasi ya kuweza kuhudhuria ile ibada ambayo itafanyika pale kesho. Asante sana mheshimiwa Spika.

Hon. Peru: Asante sana mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii. Tumetoka mapumzikoni na wakati umefika kwa Bunge hili tuweze kufanyia wana Kilifi kazi. Kazi ile hatutaweza kuifanya hapa Bungeni kama majina yale ambayo yameletwa mbele ya Bunge hili hayataweza kupitishwa. Kulingana na kazi waliyoifanya kipindi cha nyuma ni bora, tunajua ni kazi njema wamefanya kwa hivyo tuwapatie awamu nyengine ili waendeleo kutufanyia kazi ile tukiendelea kuhudumia wananchi wa Kilifi.

Vile vile, Hayati Mtukufu Rais Daniel Arap Moi ameongoza nchi hii miaka 24 akihimiza *Peace, Love and Unity* na tumeona siku tatu ziliwekwa ili wana Kenya wakaweze kumpatia mkono wa buriani Hayati Rais Daniel Arap Moi. Ningependa kumuunga mkono kakangu Hassan na mheshimiwa Naibu wa Spika vile vile kuwa ingawa wana Kilifi hatujapata nafasi ya kuenda kumpatia mkono wa kwaheri Rais yule marehemu lakini kesho ni siku ambayo imewekwa ni *Public Holiday* na kutakuwa na ibada. Hivyo basi namuunga mkono Naibu wa Spika kwamba wanakilifi hata kama sio wote lakini sisi tumechaguliwa kuwakilisha Kilifi Kaunti nzima. Kwa hivyo, Bunge hili itakuwa ni bora sana...na hatujachelewa, nahimiza hatujachelewa na yote

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

yanawezekana kuwa kesho tuwe tuko kule tumpatie mkono wa kwaheri Rais wetu mstaafu. Asanteni.

The Speaker (Hon. Kahindi): So, is the Motion about adopting the names or the burial?

(Laughter)

You are changing the Business in the Order Paper. Yes, hon. Mwamtsi?

Hon. Mwamtsi: Mr. Speaker, thank you and happy New Year to each one of us as the year has started and we are meeting for the very first time. As I stand here, I do support the list of names that has been forwarded to sit in running of the House Business Committee. Secondly, although as you have put it, it was not part of the Motion but as they say when a big tree falls the birds will scatter. As a country we are in the period of mourning and as the Bible says Happy are those who mourn while others are mourning. So, may I reiterate what has been said by my colleagues here; we cannot hide our heads under the sun as if nothing is happening. As part of the Republic of Kenya, I think it is important that we associate ourselves with what is happening. So, I do support the issue of facilitating Members Mr. Speaker to go give a hand of *kwaheri* to Mzee. Thank you.

(Question put and agreed)

ADJOURNMENT

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Members, in the absence of any other Business in the Order Paper, I move to adjourn the House. Thank you very much.

The House rose at 2.52 p.m.